

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

684

VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA

Muda: Saa 3


Ijumaa, 11 Mei 2018 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



1



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Taja kanuni nne za uchoraji picha kutokana na vitu halisi.
2. Kwa kutumia hoja mbili, fafana kwa ufupi namna ya kupausha rangi za maji.
3. Kwa kutumia hoja mbili, tofautisha kati ya mbinu shirikishi na mbinu shirikishi kiasi.
4. (a) Eleza maana ya neno Ufinyanzi.
(b) Orodhesha misingi miwili ya Ufinyanzi.
5. Ainisha mbinu nne zinazotumika katika kuwafundisha watoto wa Elimu ya Awali mada ya usimulizi wa hadithi.
6. Bainisha sifa nne za maumbo ya msingi katika uundaji.
7. (a) Eleza maana ya neno kupiga chapa.
(b) Taja vifaa vinne vinavyotumika katika kuchapa maumbo kwa kusugua.
8. Orodhesha faida nne za kutumia onesho mbinu katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya "Uchapaji" kwa watoto wa Elimu ya Awali.
9. Taja mbinu nne za utoaji sauti katika kuimba.
10. Kwa kifupi, eleza maana ya dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa watoto wa Elimu ya Awali;
(a) Njia (c) Zana
(b) Mbinu (d) Makunzi

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka katika sehemu hii.

11. "Vitendo vya Kujifunza Sanaa ni somo la vitendo zaidi kuliko nadharia." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja sita.
12. Fafanua mambo sita ya kuzingatia ili muigizaji aweze kufanikiwa katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.
13. Kwa kutumia hoja tano, oneshwa umuhimu uliopo kwa watoto wa Elimu ya Awali kujifunza dhana ya uundaji.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Fafanua faida sita za tathmini tamati katika somo la Vitendo vya Kujifunza Sanaa.
15. Eleza changamoto tano za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sanaa katika shule za Elimu ya Awali.
16. Kwanini ni muhimu kwa mwalimu kufanya maandalizi kabla ya ufundishaji na ujifunzaji wa dhana ya kuchapa maumbo? Toa sababu tano.